

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI



TANGAZO LA ZABUNI


28/12/2018

LGA/073/2018/19/MBZ/ED/02

Kwa: wananchi wote;

MWALIKO WA KAZI YA UFUNDI WA KUTENGENEZA MADAWATI

1. Halmashauri ya wilaya ya Mbozi inawakaribisha mafundi wenye vigezo kutuma maombi ya zabuni ya kazi ya ufundi wa kutengeneza madawati ya wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari za Halmashauri ya Wilaya Mbozi.
2. Halmashauri itawapatia mafundi malighafi za ufundi ambazo ni mbao, misumari, gundi na ramani ya dawati .
3. Muombaji awe mzoefu na pia awe na vifaa vya ufundi (zana) vya kufanyia kazi ambavyo ni kama nyundo na msumeno .
4. Waombaji watakaokidhi vigezo na kupewa mikataba na Halmashauri watalipwa kutokana na idadi ya madawati watakayotengeneza na yaliyokidhi viwango vilivyokubalika.
5. Waombaji wajaze gharama (kiasi cha bei) za ufundi kwa dawati moja watakalotengeneza.
6. Barua za maombi ziwasilishwe, katika ofisi za Manunuzi na Ugavi wilaya, eneo la Bomani.
7. Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Jumatano, Tarehe 02/01/2019 saa 4:00 asubuhi. Barua zitakazofika baada ya muda huo **hazitapokelewa**.
8. Mafundi wote watakaokuwa wameomba wafike katika ofisi ya idara ya Ujenzi iliyopo katika karakana ya ya Halmashauri ya Wilaya Mbozi kata ya Ichenjezya katika mji mdogo wa Vwawa, Siku ya Jumatano, Tarehe 02/01/2019, saa 4:30 asubuhi kwa ajili ya kufanyiwa usaili.
9. Barua za maombi ziandikwe "YAH: MAOMBI YA KAZI YA UFUNDI WA KUTENGENEZA MADAWATI". Barua hizo zielekezwe kwa: **Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Mbozi, S.L.P 3, Mbozi.**


Kazimbaya A. Makwega
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MBOZI

**DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
MBOZI**